

KUMB: PPR/19 - 07/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA PETROLI
KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 JULAI 2019**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Julai 2019**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya **Dar es Salaam**, zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Juni 2019. Kwa mwezi Julai 2019, bei za rejareja za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 40/lita (sawa na asilimia 1.72), Shilingi 11/lita (sawa na asilimia 0.49) na Shilingi 13/lita (sawa na asilimia 0.58), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kwa Shilingi 40.33/lita (sawa na asilimia 1.81) na Shilingi 10.94/lita (sawa na asilimia 0.52) na Shilingi 12.61/lita (sawa na asilimia 0.61), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, punguzo la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salaam linatokana na kushuka kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS premiums*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (b) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga nazo zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Juni 2019. Wakati huo huo, bei za Mafuta ya Taa hazijabadilika kwa sababu hakuna shehena ya bidhaa hiyo iliyopokelewa nchini kupitia bandari ya Tanga kwa mwezi wa Juni 2019. Kwa mwezi Julai 2019, bei za rejareja za Petroli na Dizeli **kwa Mikoa ya Kaskazini** (Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Manyara) zimepungua kwa Shilingi 64/lita (sawa na asilimia 2.69) na Shilingi 69/lita (sawa na asilimia 2.98), mtawalia. Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli na Dizeli zimepungua kwa Shilingi 64.10/lita (sawa na asilimia 2.83) na Shilingi 68.40/lita (sawa na asilimia 3.14), mtawalia. Kwa kiasi kikubwa, punguzo la bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Tanga linatokana na kushuka kwa bei za mafuta hayo katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS premiums*) kama inavyoonekana katika **Jedwali C**.
- (c) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Juni 2019. Kwa mwezi Julai 2019, bei za rejareja za Petroli **kwa Mikoa ya Kusini** (Lindi, Mtwara na Ruvuma) zimeongezeka kwa Shilingi 24/lita (sawa na asilimia 1.03) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 42/lita (sawa na asilimia 1.79). Vilevile, ikilinganishwa na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla za Petroli zimeongezeka kwa Shilingi 23.68/lita (sawa na asilimia 1.09) wakati bei za Dizeli zimepungua kwa Shilingi 41.47/lita (sawa na asilimia 1.89). Kwa kiasi kikubwa, mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la ndani kwa mafuta yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Mtwara yanatokana na punguzo la gharama za usafirishaji (*BPS Premiums*) na ongezeko la bei za mafuta hayo katika soko la dunia

kutokana na kuwa shehena ya awali ya mafuta ya Petroli iliyokuwepo katika bandari ya Mtwara ilipokelewa mwezi Aprili 2019 kwa bei za mafuta za soko la dunia za mwezi Machi 2019 ambazo zilikuwa ni ndogo ikilinganishwa na bei za mafuta katika soko la dunia za mwezi Mei 2019 zilizotumika kukokotoa bei ya sasa. Aidha, kwa kuwa hakuna Mafuta ya Taa yaliyopokelewa katika bandari ya Mtwara, wamiliki wa vituo vya mafuta katika mikoa tajwa wanashauriwa kununua mafuta hayo kutoka Dar es Salaam na hivyo bei za rejareja za Mafuta ya Taa kwa mikoa hiyo zinatokana na gharama za mafuta hayo kutokea Dar es Salaam na kusafirishwa hadi mkoa husika.

- (d) EWURA inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (e) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (f) **Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo zisivuke bei kikomo (*price cap*) kama ilivyokokotolewa na kanuni (*formula*) iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 163 la mwezi Aprili 2018 na Gazeti la Serikali Na. 269 la mwezi Juni 2018.****
- (g) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (h) Wauzaji wa mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa risiti za mauzo kutoka kwenye mashine za EFPP (*Electronic Fiscal Pump Printers*) na Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo za malipo zitatumika kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya aidha kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora kinachofaa, na pia, risiti hizo zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya mafuta ya petroli.

JEDWALI A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta Ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,312	2,210	2,167
Arusha	2,382	2,291	2,286

Arumeru (Usa West)	2,382	2,291	2,286
Karatu	2,400	2,309	2,304
Longido	2,393	2,302	2,297
Monduli	2,387	2,296	2,291
Monduli-Makuyuni	2,392	2,301	2,296
Ngorongoro (Loliondo)	2,466	2,375	2,371
Pwani (Kibaha)	2,317	2,214	2,172
Bagamoyo	2,323	2,221	2,178
Chalinze Junction	2,326	2,224	2,181
Chalinze (Msata)	2,331	2,228	2,186
Kibiti	2,333	2,230	2,188
Kisarawe	2,319	2,217	2,174
Mkuranga	2,322	2,219	2,177
Rufiji	2,340	2,237	2,195
Dodoma	2,371	2,268	2,226
Bahi	2,378	2,276	2,233
Chamwino	2,366	2,264	2,221
Chemba	2,398	2,295	2,253
Kondoa	2,404	2,301	2,259
Kongwa	2,368	2,266	2,223
Mpwapwa	2,372	2,270	2,227
Mtera (Makatopora)	2,390	2,287	2,245
Geita	2,478	2,375	2,333
Bukombe	2,467	2,364	2,322
Chato	2,499	2,396	2,354
Mbogwe	2,516	2,413	2,371
Nyang'hwale	2,493	2,390	2,348
Iringa	2,376	2,274	2,231
Ismani	2,382	2,279	2,237
Kilolo	2,381	2,278	2,236
Mufindi (Mafinga)	2,386	2,284	2,242
Kagera (Bukoba)	2,528	2,425	2,383
Biharamulo	2,502	2,399	2,357
Karagwe (Kayanga)	2,544	2,442	2,399
Kyerwa (Ruberwa)	2,550	2,447	2,405
Muleba	2,528	2,425	2,383
Ngara	2,516	2,413	2,371
Misenyi	2,536	2,434	2,391
Katavi (Mpanda)	2,520	2,418	2,375
Mlele (Inyonga)	2,502	2,399	2,357
Mpimbwe (Majimoto)	2,513	2,410	2,368
Kigoma	2,544	2,441	2,399
Uvinza (Lugufu)	2,556	2,453	2,411
Buhigwe	2,533	2,430	2,388
Kakonko	2,501	2,398	2,356
Kasulu	2,530	2,427	2,385
Kibondo	2,508	2,405	2,363
Kilimanjaro (Moshi)	2,371	2,280	2,276

Hai (Bomang'ombe)	2,375	2,284	2,279
Mwanga	2,364	2,273	2,269
Rombo (Mkuu)	2,388	2,297	2,292
Same	2,358	2,267	2,262
Siha (Sanya Juu)	2,378	2,287	2,282
Lindi	2,336	2,290	2,226
Lindi-Mtama	2,341	2,295	2,244
Kilwa Masoko	2,360	2,314	2,201
Liwale	2,372	2,326	2,247
Nachingwea	2,356	2,310	2,255
Ruangwa	2,362	2,317	2,257
Manyara (Babati)	2,416	2,325	2,320
Hanang (Katesh)	2,426	2,335	2,331
Kiteto (Kibaya)	2,431	2,340	2,335
Mbulu	2,429	2,338	2,333
Simanjiro (Orkasumet)	2,448	2,357	2,352
Mara (Musoma)	2,491	2,388	2,346
Musoma Vijijini (Busekela)	2,532	2,429	2,387
Rorya (Ingirijuu)	2,500	2,397	2,355
Rorya (Shirati)	2,535	2,432	2,390
Bunda	2,482	2,379	2,337
Bunda (Kisorya)			
Butiama	2,488	2,385	2,343
Serengeti (Mugumu)	2,537	2,434	2,392
Tarime	2,502	2,399	2,357
Tarime (Kewanja/Nyamongo)	2,507	2,404	2,362
Mbeya	2,419	2,317	2,274
Chunya	2,429	2,326	2,284
Chunya (Makongolosi)	2,443	2,340	2,298
Kyela	2,435	2,332	2,290
Mbarali (Rujewa)	2,404	2,301	2,259
Rungwe (Tukuyu)	2,428	2,326	2,283
Morogoro	2,337	2,235	2,192
Mikumi	2,353	2,250	2,208
Kilombero (Ifakara)	2,375	2,272	2,230
Kilombero (Mlimba)	2,398	2,295	2,253
Kilombero (Mngeta)	2,387	2,284	2,242
Ulanga (Mahenge)	2,386	2,283	2,241
Malinyi	2,396	2,293	2,251
Kilosa	2,356	2,253	2,211
Gairo	2,356	2,253	2,211
Mvomero (Wami Sokoine)	2,348	2,245	2,203
Mvomero (Sanga Sanga)			
Turiani	2,362	2,260	2,217
Mtwara	2,323	2,277	2,240
Nanyumbu (Mangaka)	2,359	2,313	2,289
Masaki	2,339	2,293	2,265
Newala	2,343	2,298	2,272

Tandahimba	2,337	2,291	2,265
Nanyamba	2,337	2,291	2,265
Mwanza	2,462	2,360	2,317
Kwimba	2,480	2,378	2,335
Magu	2,471	2,368	2,326
Misungwi	2,457	2,354	2,312
Sengerema	2,495	2,392	2,350
Ukerewe	2,522	2,419	2,377
Njombe	2,405	2,302	2,260
Njombe (Kidegembye)	2,425	2,323	2,280
Ludewa	2,443	2,340	2,298
Makambako	2,397	2,294	2,252
Makete	2,436	2,333	2,291
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,403	2,300	2,258
Rukwa (Sumbawanga)	2,485	2,383	2,340
Sumbawanga Rural (Mtowisa)	2,485	2,383	2,340
Kalambo (Matai)	2,492	2,390	2,348
Nkasi (Namanyeke)	2,499	2,396	2,354
Ruvuma (Songea)	2,408	2,362	2,291
Mbinga	2,421	2,375	2,324
Namtumbo	2,399	2,353	2,320
Nyasa (Mbamba Bay)	2,446	2,400	2,335
Tunduru	2,373	2,328	2,350
Shinyanga	2,441	2,338	2,296
Kahama	2,455	2,352	2,310
Kishapu	2,470	2,367	2,325
Ushetu (Nyamilangano)	2,472	2,370	2,328
Simiyu (Bariadi)	2,483	2,380	2,338
Busega (Nyashimo)	2,476	2,373	2,331
Itilima (Lagangabilili)	2,486	2,383	2,341
Maswa	2,474	2,371	2,329
Meatu (Mwanhuzi)	2,481	2,378	2,336
Singida	2,403	2,300	2,258
Iramba	2,415	2,312	2,270
Manyoni	2,387	2,285	2,243
Ikungi	2,399	2,296	2,254
Mkalama (Nduguti)	2,428	2,325	2,283
Songwe (Vwawa)	2,429	2,326	2,284
Songwe (Mkwajuni)	2,436	2,333	2,291
Ileje	2,433	2,330	2,288
Momba (Chitete)	2,438	2,335	2,293
Tunduma	2,433	2,330	2,288
Tabora	2,467	2,364	2,322
Igunga	2,420	2,318	2,276
Kaliua	2,486	2,383	2,341
Ulyankulu	2,480	2,377	2,335
Nzega	2,431	2,328	2,286
Sikonge	2,478	2,376	2,333

Urambo	2,480	2,377	2,335
Uyui	2,468	2,365	2,323
Tanga	2,325	2,234	2,229
Handeni	2,346	2,255	2,250
Kilindi	2,361	2,270	2,265
Korogwe	2,337	2,246	2,241
Lushoto	2,347	2,256	2,251
Mkinga (Maramba)	2,332	2,241	2,236
Muheza	2,330	2,239	2,234
Pangani	2,332	2,241	2,236

JEDWALI B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,188.02	2,085.23	2,043.75

Bei za Jumla - TANGA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,200.82	2,109.70	2,105.56

Bei za Jumla - MTWARA	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Bei Kikomo	2,198.29	2,152.42	-----

JEDWALI C: SABABU ZA MABADILIKO YA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI

BANDARI YA DAR ES SALAAM

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 18.516/Tani	Punguzo la Dola 8.471/Tani	Ongezeko la Dola 8.135/Tani
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Punguzo la Dola 16.813/Tani	Punguzo la Dola 2.323/Tani	Punguzo la Dola 9.207/Tani

BANDARI YA TANGA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Punguzo la Dola 18.516/Tani	Punguzo la Dola 5.331/Tani	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Punguzo la Dola 26.158/Tani	Punguzo la Dola 20.250/Tani	----

BANDARI YA MTWARA

	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mabadiliko ya Bei za mafuta katika soko la dunia	Ongezeko la Dola 48.643/Tani	----	----
Mabadiliko ya gharama za usafirishaji (BPS premiums)	Punguzo la	Punguzo la	----

usafirishaji (<i>BPS premiums</i>)	Dola 20.520/Tani	Dola 10.560/Tani	
--------------------------------------	------------------	------------------	--

**JEDWALI D: BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA ZILIZOTUMIKA
KUKOKOTOA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA NDANI**

	Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Mafuta yalipokelewa mwezi wa:	DSM	Juni 2019	Juni 2019	Juni 2019
	Tanga	Juni 2019	Juni 2019	Desemba 2018
	Mtwara	Juni 2019	Mei 2019	n/a
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa mwezi:	DSM	Mei 2019	Mei 2019	May 2019
	Tanga	Mei 2019	Mei 2019	Novemba 2018
	Mtwara	Mei 2019	Aprili 2019	----
Wastani wa bei za mafuta katika soko la dunia kwa miezi inayoonekana hapo juu inalinganishwa na wastani wa bei za mwezi:	DSM	Aprili 2019	Aprili 2019	Aprili 2019
	Tanga	Aprili 2019	Aprili 2019	----
	Mtwara	Machi 2019	----	----

**Nzinyangwa E. Mchany
KAIMU MKURUGENZI MKUU
EWURA**